NMB
Karibu yako

Miaka 25

# MKUTANO MKUU WA MWAKA 2023

SAFARI YA MAFANIKIO



## 23.1 TAARIFA YA KUITISHA MKUTANO NA AKIDI

Wanahisa wanaombwa kuzingatia taarifa iliyotolewa kulingana na Kanuni ya 51 ya Kanuni za Kampuni inayohusu uitishaji wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa.

Wanahisa wanaombwa kuzingatia kuwa, akidi kwa mujibu wa Kanuni ya 55 ya Kanuni za Kampuni ni idadi ya wanahisa wasiopungua 25 wanaomiliki hisa zisizopungua asilimia 51 au wawakilishi wenye sifa hizo pamoja na mwakilishi mmoja aliyeidhinishwa kutoka kwa wanahisa wanaomiliki angalau asilimia 25 ya hisa zote.

Wanahisa wanatakiwa kuhudhuria kikao ndani ya nusu saa kabla ya muda uliopangwa kuanza Mkutano. Vinginevyo, Mkutano utaahirishwa.

## 23.2 KUPOKEA AJENDA

Wanahisa mnaombwa kupitisha Ajenda za Mkutano Mkuu wa 23 kama zilivyowasilishwa.

# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 23 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka (23) wa Wanahisa wa Benki ya NMB utafanyika kwa njia ya mtandao (kidijitali) siku ya Ijumaa tarehe 2 Juni 2023 kuanzia saa 4 asubuhi. Agenda zitakuwa kama ifuatavyo:**

23.1 MATANGAZO NA AKIDI

23.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

23.3 KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA 22 ULIOFANYIKA TAREHE 3 JUNI 2022

23.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 22 WA WANAHISA

23.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022

23.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2022

23.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI

23.8 KUJIUZULU NA UTEUZI WA WAKURUGENZI

23.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DISEMBA 2023

23.10 MENGINEYO

## 23.3 KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA 22 ULIOFANYIKA TAREHE 3 JUNI 2022

**Wasilisho:**

Wanahisa mnaombwa kupokea na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 22 uliofanyika tarehe 3 Juni 2022 kama kumbukumbu sahihi ya Mkutano huo kwa kuazimia ifuatavyo.

***"AZIMIO LA 1/2023:***
***Imeazimiwa kwamba Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Ishirini na Mbili (22) uliofanyika tarehe 3 Juni 2022 ni kumbukumbu sahihi."***

# MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE TAREHE 3 JUNI 2022 SAA 4.00 ASUBUHI.

## WALIOHUDHURIA

MWENYEKITI

Dkt. Edwin P. Mhede - Mwenyekiti

## WANAHISA WAKUBWA

1. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Ikiwakilishwa na Bw. Elikana Mtumweni (Mwakilishi wa Msajili wa Hazina)
2. Arise B.V. - Ikiwakilishwa na Bw. Hugo Azevedo
3. Wanahisa wengine - (Orodha Imeambatanishwa)

## WAKURUGENZI

1. Bw. Hendrik Reisinger - Mkurugenzi
2. Bw. George Mandepo - Mkurugenzi
3. Bw. Juma Kisaame - Mkurugenzi
4. Bw. Benson Mahenya - Mkurugenzi
5. Bi. Theresia Pascal - Mkurugenzi

## SEKRETARIATI

Bi. Consolatha Mosha - Kaimu Katibu

## WALIOKARIBISHWA (UONGOZI WA BENKI)

1. Bi. Ruth Zaipuna - Afisa Mtendaji Mkuu
2. Bw. Aziz Chacha - Mhazini
3. Bw. Alfred Shao - Afisa Mkuu Biashara, Wateja Wakubwa
4. Bw. Filbert Mponzi - Afisa Mkuu Biashara, Wateja wa Kati na Wadogo
5. Bw. Juma Kimori - Afisa Mkuu Fedha
6. Bi. Nenyuata Mejooli - Afisa Mkuu Huduma Shirikishi
7. Bw. Emmanuel Akoonay - Afisa Mkuu Rasilimali Watu
8. Bw. Daniel Mbotto - Afisa Mkuu Mikopo
9. Bw. Hance Onesmo - Kaimu Afisa Mkuu Teknolojia na Mabadiliko ya Kidijitali
10. Bw. Oscar Nyirenda - Kaimu Afisa Mkuu Udhibiti wa vihatarishi na Ufuatiliaji

# MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE TAREHE 3 JUNI 2022 SAA 4.00 ASUBUHI.

## 22.1 TAARIFA NA AKIDI

- Mwenyekiti alifungua mkutano na kuwakaribisha Wanahisa, Wakurugenzi na Menejimenti ya Benki ya NMB kwenye Mkutano Mkuu wa 22 wa Wanahisa wa Benki ya NMB.

- Baada ya kutoa taarifa kwamba Fomu za uwakilishi zimepokelewa kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Arise B.V ilikubalika kwamba akidi imekamilika ili kuanza Mkutano Mkuu wa 22 kulingana na matakwa ya Kanuni ya 55 ya Kanuni za Kampuni.

## 22.2 KUPOKEA AJENDA

- Kwa kuwa hakukuwa na mabadiliko yoyote, ajenda za Mkutano zilipokelewa.

## 22.3 KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA (21) WA MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 4 JUN1, 2021 SAA 4.00 ASUBUHI KWA NJIA YA MTANDAO

- Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Ishirini na Moja ulithibitishwa kuwa ni kumbukumbu sahihi ya Mkutano uliopita na ukasainiwa na Mwenyekiti na Kaimu Katibu wa Kampuni.

***AZIMIO NA. 1/2022***

***"Ilikubalika kwamba muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Ishirini na Moja uliofanyika tarehe 4 Juni, 2021 ni sahihi."***

## 22.4 YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA WA WANAHISA

- Hapakuwa na yatokanayo kwenye Mkutano Mkuu wa Wanahisa wa Ishirini na Moja.

## 22.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUIDHINISHA TAARIFA YA WAKURUGENZI NA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2021

- Afisa Mtendaji Mkuu aliwaarifu Wanahisa mafanikio na mwenendo wa Benki, Historia, mabadiliko na muundo wa umiliki wa hisa viliainishwa.

- Wanahisa waliarifiwa juu ya mafanikio makubwa ya benki yakithibitishwa na matokeo ya utendaji wa Benki kwa mwaka ulioshia tarehe 31 Disemba 2021.

## MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE TAREHE 3 JUNI 2022 SAA 4.00 ASUBUHI.

Hii inaonesha nia thabiti ya Bodi na Menejimenti katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati (2025). Mwaka 2021 ulikuwa mwaka wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati 2025.

- Mwaka 2021, Benki ilifanikiwa kuongeza idadi ya wateja na kufika milioni 5 kutoka wateja milioni 4, iliongeza idadi ya mashine za kutolea fedha (ATM) kufikia 755 kutoka 753, iliongeza idadi ya Mawakala mpaka 10,194 kutoka 8,410. Idadi ya matawi iliendelea kuwa 226 na hii ilichangiwa na Benki kuunganisha baadhi ya matawi yaliyopo karibu na kufungua matawi mapya maeneo yenye uhitaji zaidi. Benki iliendelea kuwekeza kwenye njia mbadala ya utoaji huduma za kibenki kama ATM na Wakala ili kufikisha huduma za kibenki kwa urahisi kwa wateja. Idadi ya wafanyakazi iliongezeka mpaka kufikia 3,482 mwaka 2021 kutoka 3,465 mwaka 2020.

- Mwaka 2021, Benki ya NMB ilitambuliwa na kutunukiwa tuzo saba za kimataifa ikiwemo tuzo ya Euromoney ya Ubora, ikiitambua benki ya NMB kama Benki bora Tanzania (kwa miaka tisa mfululizo) na tuzo kutoka Jarida la Global Finance ikiitambua benki ya NMB kama benki salama zaidi Tanzania.

- Pia mwaka 2021, benki ya NMB ilitambuliwa na kupewa tuzo na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikiitambua kama mlipa kodi mkubwa zaidi kwenye sekta ya fedha na pia mlipa kodi mkubwa namba tatu kwa ujumla nchini.

- Benki iliendelea kuimarisha utendaji wake kwa kuwa benki kiongozi kwenye sekta ya fedha kwa kupata faida baada ya kodi ya TZS 290 Bilioni hivyo kumiliki asilimia 40 ya faida ya sekta na kuwa na uwiano wa gharama kwa mapato wa asilimia 46.

- NMB iliendelea kuhakikisha inajitolea kwa jamii ambapo kwa mwaka 2021, ilizindua taasisi ya NMB Foundation yenye dhumuni la kusaidia sekta za Elimu, Afya, Mazingira, Ujasiriamali na Kilimo.

- Kama benki kiongozi, NMB ina jukumu la kuhakikisha watu wengi zaidi wanaingia kwenye sekta rasmi ya kibenki na ili kufanikisha azma hii benki iliwekeza kwenye mifumo ya kidigitali ambapo benki ilizindua masuluhisho matatu ambayo ni Mshiko Fasta (mikopo midogo mpaka TZS 500,000/=), NMB Pesa Wakala na Lipa Mkononi.

- Benki imeendelea kuwekeza kidigitali kwenye Mfumo wa Uendeshaji wa Benki (Core Banking System), Mfumo wa Usimamizi wa Mikopo (Loan Management System), Usimamizi wa Taarifa (Master Data Management) na Mfumo wa Usimamizi wa Mahusiano na Wateja (Customer Relationship Management System).

## MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE TAREHE 3 JUNI 2022 SAA 4.00 ASUBUHI.

- Uendelevu wa Benki uliendelea kuonekana mwaka 2021 ambapo Benki ilijitolea kwa jamii kiuchumi na kwenye mazingira. Benki ilitoa zaidi ya madawati 32,000 ya shule, vituo vya afya 6,000 vilikabidhiwa vifaa vya matibabu, wakulima 10,000 waliwezeshwa kupitia programu za kilimo na TZS 4.3 Trilioni zilitolewa kwa ajili ya wafanyabiashara wa kati na wadogo, kilimo na watu binafsi.

- Benki iliongeza thamani kwa washirika wake kama ifuatavyo; TZS 187 Bilioni ilitumika kwa wafanyakazi wa benki, TZS 269 Bilioni ililipwa kama kodi za serikali; TZS 96.7 Bilioni ilitengwa kama gawio kwa wanahisa (kiasi hiki kinafanya jumla ya gawio kwa miaka mitatu mfululizo kuwa TZS 213 Bilioni) na TZS 227 Bilioni ilitumika kwa ajili ya upanuzi na uwekezaji ndani ya benki.

- Katika mwaka 2021 benki ya NMB ilirekodi jumla ya mapato ya TZS 982 Bilioni ambalo ni ongezeko la 18% mwaka hadi mwaka na gharama za uendeshaji ziliongezeka mpaka kufikia TZS 445 Bilioni ikiwa ni ongezeko la 9%.

- Tengo la mikopo chechefu lilipungua kwa 5% mwaka hadi mwaka kutoka TZS 119 Bilioni mwaka 2020 mpaka TZS 113 Bilioni mwaka 2021. Hii iliashiria ongezeko la ubora wa mikopo.

- Faida kabla ya kodi ilikuwa TZS 414 Bilioni ambapo ni ongezeko la 40% mwaka hadi mwaka na faida baada ya kodi ilikuwa TZS 290 Bilioni ambapo ni ongezeko la 41% mwaka hadi mwaka ikilinganishwa na mwaka 2020. Afisa Mtendaji Mkuu alifafanua kuwa utendaji mzuri wa benki kwa mwaka 2021 ulichangiwa na ongezeko la mapato yaliyotokana na mauzo na utumiaji wa njia mbadala za kibenki, ubora wa mikopo na mipango ya kudhibiti gharama.

- Mikopo iliongezeka kwa 13% mwaka hadi mwaka, amana za wateja ziliongezeka kwa 25% mwaka hadi mwaka, jumla ya mali iliongezeka kwa 23% mwaka kwa mwaka, mtaji daraja la kwanza ilikuwa 23.8% na mtaji wa jumla ulikuwa 24.6%.

- Afisa Mtendaji Mkuu alitoa pia taarifa fupi ya uendeshaji wa robo ya kwanza ya mwaka 2022. Mikopo iliongezeka na kufikia TZS 4.6 Trilioni ikiwa ni ongezeko la 13% mwaka hadi mwaka. Amana za wateja ziliongezeka na kufikia TZS 6.6 Trilioni ikiwa ni ongezeko kwa 25% mwaka hadi mwaka, jumla ya mali iliongezeka mpaka TZS 8.7 Trilioni ikiwa ni ongezeko la 23% mwaka hadi mwaka, mtaji wa wanahisa uliongezeka mpaka TZS 1,351 Trilioni ikiwa ni ongezeko la 20% mwaka hadi mwaka. Benki ilirekodi jumla ya mapato ya TZS 275 Bilioni kwa Robo ya kwanza ya mwaka 2022 ikiwa ni ongezeko la 23% mwaka hadi mwaka, gharama za uendeshaji ziliongezeka mpaka TZS

## MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE TAREHE 3 JUNI 2022 SAA 4.00 ASUBUHI.

116 Bilioni ikiwa ni ongezeko la 8% mwaka hadi mwaka. Faida kabla ya kodi ilikuwa TZS 144 Bilion ikiwa ni ongezeko la 55% na faida baada ya kodi ilikuwa TZS 101 Bilioni ikiwa ni ongezeko la 54% mwaka hadi mwaka. Robo ya kwanza ya mwaka 2022 iliashiria muelekeo mzuri wa mwaka 2022 na kuendelea mbele.

### MASWALI YA WANAHISA YALIJIBIWA KAMA IFUATAVYO:-

- **Kuchelewa kwa Kitabu cha Mkutano Mkuu na Taarifa ya Mwaka**
  Wanahisa walifahamishwa maoni yao yamepokelewa na kwenda mbele kitabu cha Mkutano Mkuu na Taarifa ya Mwaka zitatolewa kwa wanahisa wiki mbili kabla ya kikao cha wanahisa kupitia njia rasmi za mawasiliano ikiwepo tovuti ya benki ya NMB.

- **Kiasi kikubwa cha Mikopo Chechefu**
  Wahahisa walijulishwa kwamba benki ikitoa mikopo zingatio kubwa huwa ni uwezo wa mkopaji kurejesha fedha hizo kwa kuangalia mzunguko wa fedha wa mkopaji. Mikopo chechefu ni takwa la kisheria ambalo linatakiwa lihesabiwe na kuwasilishwa kwa mthibiti. Benki huchukua dhamana kwa mikopo inayotoa na endapo mkopaji atashindwa kurejesha mkopo, benki itakuwa na haki ya kuuza dhamana kulingana na taratibu zilizopo. Menejimenti itaendelea kufuatilia marejesho ya mikopo chechefu kwa kupitia dhamana zilizowekwa.

- **Kushughulikia Malalamiko matawini**
  Taratibu za kuwasilisha malalamiko zipo na hivyo Menejimenti itasisitiza matawi yote kuelekeza wateja wetu juu ya hizi taratibu na kushughulikia malalamiko hayo kwa haraka.

- **Uwezekano wa Hati Fungani na Hisa kutumika kama dhamana ya mikopo**
  Wanahisa walifahamishwa kuwa benki ya NMB inapokea hisa na Hati Fungani kama dhamana kwa ajili ya mikopo na uongozi wa Benki ya NMB utaendelea kuelimisha matawi yote juu ya hili. Hata hivyo, ilifafanuliwa kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 26(1) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Kifedha za Mwaka 2006 (na marekebisho yake), benki ya NMB haiwezi kupokea Hisa za NMB kama dhamana kwa mikopo inayoitoa.

- **Kudaiwa nyaraka mara kwa mara kila wakati mteja anapofungua akaunti nyingine**
  Uongozi wa benki ulipokea changamoto hiyo na umejipanga kufanya marekebisho kwa kuhifadhi kikamilifu taarifa za wateja kupitia uwekezaji wetu wa kidigitali ili kurahisisha mchakato wa kufungua akaunti huku ikiendelea kuzingatia mahitaji ya kumjua mteja.

## MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE TAREHE 3 JUNI 2022 SAA 4.00 ASUBUHI.

- **Ukomo wa kiasi cha kutoa fedha katika mashine za kutolea fedha kielektroniki (ATM)**
  Wanahisa walifahamishwa kuwa ukomo huu umewekwa kwenye njia zote mbadala za kutolea fedha kwa sababu za kiusalama zaidi. Aidha, mashine zote za kutolea fedha kielektroniki zimetengenezwa na ukomo wa kutoa noti zisizozidi arobaini kwa mkupuo mmoja.

- **Kuvutia akaunti za amana za kudumu pamoja na akaunti nyingine zinazotoa riba**
  Kama benki tuna akaunti tofauti tofauti kama current akaunti ambayo haitoi riba kwa mteja lakini kuna akaunti nyingine zinazotoa riba kama bonus akaunti na fixed akaunti (inategemea na makubaliano baina ya benki na mteja ambapo itategemea na kiwango cha fedha na muda wake). Benki itaendaelea kutoa elimu kwa wanahisa wake pamoja na wateja wengine juu ya faida ya kila akaunti.

- **Utoaji wa Mikopo ya Kilimo**
  Wanahisa walikumbushwa kuwa mwaka 2021 benki ilitoa TZS 100 Bilioni mahususi kwa sekta ya kilimo ambapo mikopo yenye riba ya 9% ilichukuliwa kwa kasi kubwa sana hivyo kupelekea benki kuongeza kiasi kingine cha TZS 100 Bilioni kwa ajili ya sekta ya kilimo. Pamoja na haya Benki itaendelea kutoa kipaumbele kwenye Sekta ya Kilimo.

- **Kutoa zabuni za ujenzi wa matawi kwa mafundi wa eneo husika ambapo tawi lipo**
  Ilifahamishwa kwamba kazi hizi huwa zinafuata utaratibu wa manunuzi wa benki ambapo kampuni zinazokidhi vigezo husika ndizo hupata zabuni lakini matawi yamepewa mamlaka ya kutumia mafundi wa eneo husika kwenye marekebisho madogo madogo.

- **Taarifa ya idadi ya hisa anazomiliki Mwanahisa kuainishwa kwenye kitabu cha Mkutano Mkuu**
  Benki iliahidi kuhakikisha kuwa taarifa zijazo hazitaonesha idadi ya hisa zinazomilikiwa na kila mwanahisa kwenye orodha ya mahudhurio ya Mkutano.

- **Kadirio kwenye Kiasi cha Gawio**
  - Kiwango cha gawio kilichooneshwa kwenye kitabu ni kadirio la karibu lakini wakati wa malipo gawio litalipwa lote kama inavyotakiwa.
  - Moja ya tatu (33.3%) ya faida baada ya kodi hulipwa kama gawio kwa mujibu wa Kanuni za Kampuni, hivyo mabadiliko yoyote ya kiwango hiki yatapaswa kufanyika kwenye Kanuni hizo.

- Aidha, kutangaza gawio kunaangalia pia matakwa ya Benki Kuu kuhusu kiwango maalum cha Mtaji Mkuu ambacho benki inapaswa kuwa nacho muda wote na kwa kuzingatia mipango ya upanuzi wa biashara.

- **Tofauti kubwa baina ya faida kabla ya kodi na faida baada ya kodi**
  Wanahisa walielezwa kuwa sheria imeelekeza kuwa 30% ya faida ikatwe kama kodi ambayo baada ya kupiga hesabu inaleta faida baada ya kodi ya TZS 290 Bilioni.

- **Namba ya Bure ya kuwasiliana na Huduma kwa Wateja**
  Benki iliahidi kufahamisha umma namba ya kuwasiliana na kitengo cha huduma kwa wateja bila gharama yoyote kwa mpigaji.

- **Pendekezo kuwa Wakurugenzi wa Bodi watokee vijijini**
  Ilibainishwa kuwa Wakurugenzi (Watanzania) wanatoka sehemu za vijijini na wana uelewa wa changamoto za jamii. Hata hivyo, ushauri ulitolewa kwamba mahali anapotoka mtu haipaswi kuwa kigezo pekee au cha msingi katika kuchagua Wakurugenzi wa Bodi kwa sababu wanapaswa kuwa na weledi katika fani fulani ili kuweza kushauri na kusimamia uongozi wa benki.

  Aidha, Sheria za Makampuni vimeweka wajibu juu ya wakurugenzi kulinda maslahi ya wanahisa na pia ukurugenzi wa benki ni nafasi ambayo inadhibitiwa sana hivyo wanahisa walithibitishiwa kuwa maslahi yao yanatunzwa vyema.

- Wanahisa waliipongeza bodi na uongozi wa benki kwa utendaji mzuri na matokeo mazuri kwa mwaka 2021.

- Wanahisa walipokea Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2021 kwa kupitisha azimio lifuatalo:

***AZIMIO NA. 2/2022***
***"Imeazimiwa kwamba Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2021 imepitishwa kama ilivyowasilishwa"***

## 22.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA WA FEDHA 2021

**Wanahisa walifahamishwa kwamba;**

- Bodi ya Wakurugenzi ilipendekeza gawio la TZS 193/= kwa kila hisa lilipwe kutokana na faida baada ya kodi ya TZS 290 Bilioni ya mwaka 2021.

## MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE TAREHE 3 JUNI 2022 SAA 4.00 ASUBUHI.

- Wanahisa waliidhinisha gawio la hisa la jumla ya TZS 96.7 Bilioni lilipwe kutokana na faida baada ya kodi ya mwaka 2021 kwa kupitisha Azimio lifuatalo;

*AZIMIO NA. 3/ 2022*
***"Imeazimiwa kwamba, kama ilivyopendekezwa na Wakurugenzi wa Bodi kwamba, gawio la shilingi za Kitanzania mia moja tisini na tatu (193/=) kwa kila hisa, ambayo ni jumla ya shilingi za Kitanzania 96.7 Bilioni kwa ujumla limetangazwa kwa ajili ya kipindi cha Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba 2021 na pia gawio hilo liwe limelipwa ama kabla au ifikapo tarehe 15 Juni, 2022 kwa wale wanahisa walioorodheshwa kwenye Kitabu cha Wanahisa hadi tarehe 1 Juni, 2022"***

### 22.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MAPENDEKEZO YA MALIPO YA WAKURUGENZI

- Afisa Mkuu Fedha aliwasilisha kwa Wanahisa pendekezo la mabadiliko ya malipo ya Wakurugenzi wa Bodi.

- Baada ya kuhakiki soko, Menejimenti ilipendekeza malipo ya Wakurugenzi yarekebishwe na yaongezwe kama inavyooneshwa kwenye kiambatanisho cha Kifurushi cha Stahiki za Wakurugenzi kwa mwaka 2022. Mabadiliko haya yalipendekezwa baada ya kupitia malipo ya Wakurugenzi kwenye benki nyingine na baadhi ya makampuni yalioordheshwa kwenye soko la hisa.

- Wanahisa walipitisha Azimio lifuatalo:-

*AZIMIO NA. 4/2021*
***"Imeazimiwa kwamba, kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi yarekebishwe kama inavyopendekezwa kwenye Kifurushi cha Stahiki za Wakurugenzi wa NMB mwaka 2022".***

### 22.8 KUPOKEA NA KUIDHINISHA KUJIUZULU KWA WAKURUGENZI

- Kulingana na Kanuni ya 81 ya Kanuni za Kampuni, kila mwanahisa mwenye zaidi ya 10% ya hisa katika mtaji wa hisa wa Kampuni anasathili kumteua Mkurugenzi mmoja kwa kila 10% ya hisa zake.

- Bw. Hendrick Reisinger aliyeteuliwa na ARISE B.V amekamilisha muhula wake wa miaka mitatu na hivyo ameteuliwa tena kwa muhula mwingine.

- Bi. Christine Glover ambaye aliteuliwa na ARISE B.V alijiuzulu kwenye Bodi ya Wakurugenzi tarehe 18 Januari 2022, mchakato wa kumchagua mbadala wake unaendelea, ukikamilika wanahisa wataarifiwa ili watoe idhini yao.

## MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI (22) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ULIOFANYIKA DAR ES SALAAM KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA KIMATAIFA WA JULIUS NYERERE TAREHE 3 JUNI 2022 SAA 4.00 ASUBUHI.

- Wanahisa waliombwa kukubali kuteuliwa tena kwa Bw. Hendrick Reisinger katika Bodi ya Wakurugenzi wa NMB na kujiuzulu kwa Bi. Christine Glover katika Bodi ya wakurugenzi ya NMB.

***AZIMIO NA. 5/2022***
***"Imeazimiwa kuwa Bw. Hendrick Reisinger ateuliwe tena kujiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kwa kipindi kingine cha miaka mitatu"***

***AZIMIO NA. 6/2022***
***"Imeazimiwa kuwa kujiuzulu kwa Bi. Christine Glover kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kumekubaliwa"***

- Wanahisa waliarifiwa kwamba Bw. George Mandepo aliyeteuliwa na Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania amekamilisha muhula wake wa miaka mitatu na hivyo ameteuliwa tena kwa muhula mwingine.

- Aidha, kulingana na Kanuni ya 81 ya Kanuni za Kampuni, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imemteua Bw. Aziz Dachi, kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kwa kipindi cha miaka mitatu. Bw. Dachi anachukua nafasi ya Bi. Theresia Pascal.

***AZIMIO NA. 7/2022***
***"Imeazimiwa kuwa Bw. George Mandepo ateuliwe tena kujiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kwa kipindi cha miaka mitatu"***

***AZIMIO NA. 8/2022***
***"IImeazimiwa kuwa nafasi ya Bi. Theresia Paschal kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya NMB ichukuliwe na Bw. Azizi Dachi"***

***AZIMIO NA. 9/2022***
***"Imeazimiwa kuwa Bw. Azizi Dachi ateuliwe kujiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kwa kipindi cha miaka mitatu"***

- • Wanahisa waliarifiwa kuwa Bw. Leonard Mususa na Bw. George Mulamula ambao ni Wakurugenzi huru waliochaguliwa na Umma, walijiuzulu kwenye Bodi ya Wakurugenzi tarehe 18 Januari 2022. Taratibu za uchaguzi wa Wakurugenzi wengine ziliendelea ambapo kulingana na Kanuni ya 82 ya Kanuni za Kampuni, Wakurugenzi wanaohitajika ni kutoka fani ya Tehama (IT) na kutoka fani ya Uhasibu/Ukaguzi. Bodi ya Wakurugenzi wanapendekeza na kuomba ridhaa ya uteuzi wa Bw. Ramadhani Mwikalo na Bw. Clement Mwinuka kwa ajili hiyo, mtawalia.

- • Wanahisa waliombwa kuridhia kujiuzulu kwa Bw. Leonard Mususa na Bw. George Mulamula na kuridhia kuteuliwa kwa Bw. Ramadhani Mwikalo na Bw. Clement Mwinuka katika Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kwa kipindi cha miaka mitatu.

***AZIMIO NA. 10/2022***
***"Imeazimiwa kuwa kujiuzulu kwa Bw. Leonard Mususa kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kumeridhiwa"***

***AZIMIO NA. 11/2022***
***"Imeazimiwa kuwa kujiuzulu kwa Bw. George Mulamula kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kumeridhiwa"***

***AZIMIO NA. 12/2022***
***"Imeazimiwa kuwa Bw. Ramadhani Mwikalo ateuliwe kujiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kwa kipindi cha miaka mitatu"***

***AZIMIO NA. 13/2022***
***"Imeazimiwa kuwa Bw. Clement Mwinuka ateuliwe kujiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya NMB kwa kipindi cha miaka mitatu"***

## 22.9 KUPOKEA NA KUPITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA NJE WA HESABU KWA MWAKA 2022

- Wanahisa walitaarifiwa kwamba kampuni ya wakaguzi wa nje ya PwC imekagua benki kwa vipindi viwili vya miaka mitatu mitatu na hivyo kukamilisha muda wa miaka 6 mfululizo. Kwa mujibu wa maelekezo ya Benki Kuu, PwC hawaruhusiwi kuendelea kufanya ukaguzi wa benki kwa kipindi kingine. Bodi ya Wakurugenzi iliishukuru kampuni ya PwC kwa kazi nzuri.

- Wanahisa waliombwa kupitisha uteuzi wa Kampuni ya Deloitte & Touche kuwa Wakaguzi wa nje wa NMB kwa mwaka 2022 kwa ada ya shilingi za kitanzania 593,953,000/= (pamoja na kodi) kwa kupitisha Azimio lifuatalo:

***AZIMIO NA. 14/2022***
***"Imeazimiwa kwamba kulingana na Kanuni ya 147 ya Kanuni ya Kampuni, Deloitte & Touche ambayo imeonyesha utayari wa kufanya kazi mpaka Mkutano Mkuu wa mwaka ujao wa wanahisa ambapo Mahesabu ya Mwaka unaishia 31 Disemba 2022 yatakuwa yamewasilishwa kwenye kampuni, wateuliwe kuwa Wakaguzi wa nje wa mahesabu ya kampuni kwa kipindi cha mwaka wa Fedha wa 2022 kwa ada ya Shilingi za Kitanzania 593,953,000/= (pamoja na kodi)"***

## 22.10 MENGINEYO

- Kwa kuwa hakukuwa na mengineyo, Mwenyekiti aliwashukuru Wanahisa kwa kuhudhuria mkutano na michango yao.

- Mkutano ulifungwa saa 7:00 Mchana.

KATIBU: ........................................ MWENYEKITI: ........................................

TAREHE: ........................................

| NA. | JINA LA MWANAHISA | UWAKILISHI | MWAKILISHI |
|---|---|---|---|
| 1 | NATIONAL INVESTMENTS COMPANY LIMITED | MWAKILISHI | ABDUL-HAFIDH HASSAN MARUA |
| 2 | SC (T) NOMINEE RE:STANDARD CHARTERED BANK UGANDA RE:NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND | MWAKILISHI | LEYLA DAHAL |
| 3 | AUNALI FIDAHUSSEIN RAJABALI | MWAKILISHI | FRANK LUCAS BUNUMA |
| 4 | SAJJAD FIDAHUSSEIN RAJABALI | MWAKILISHI | FRANK LUCAS BUNUMA |
| 5 | PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND | MWAKILISHI | HERMAN GOOLDUCK PATRICK |
| 6 | DUET AFRICA OPPORTUNITIES MASTER FUND IC | MWAKILISHI | STANBIC NOMINEES LIMITED |
| 7 | TCCIA INVESTMENT COMPANY LTD | MWAKILISHI | JOSEPH KAHUNGWA |
| 8 | UMOJA UNIT TRUST SCHEME | MWAKILISHI | FREDRIC PETER LUSHINGE |
| 9 | ZANZIBAR SOCIAL SECURITY FUND | BINAFSI | |
| 10 | BNYM RE FRONTAURA GLOBAL FRONTIER FUND LLC | MWAKILISHI | STANBIC NOMINEES LIMITED |
| 11 | SCB MAURITIUS A/C SANLAM CENTRE SUB SAHARAN AFRICA EQUITY MASTER FUND CLASS E | MWAKILISHI | LEYLA DAHAL |
| 12 | NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND | MWAKILISHI | GODSON KIMBI |
| 13 | MOHAMED H. WARSAME | MWAKILISHI | FRANK LUCAS BUNUMA |
| 14 | ADAM ISAELI ELINEWINGA | BINAFSI | |
| 15 | ZANZIBAR SOCIAL SECURITY FUND | BINAFSI | |
| 16 | NHC AND PPF INVESTMENT CO LTD | MWAKILISHI | KHAMIS MNDOHOLELE |
| 17 | KEBRON ANDERSON MAHOO | BINAFSI | |
| 18 | JIKIMU UNIT TRUST SCHEME | MWAKILISHI | FREDRIC PETER LUSHINGE |
| 19 | JONAS J K MASABALA | BINAFSI | |
| 20 | DEOGRATIAS POLYCARD USANGIRA | BINAFSI | |
| 21 | ROLDO LIMITED | BINAFSI | |
| 22 | UMOJA UNIT TRUST SCHEME | MWAKILISHI | FREDRIC PETER LUSHINGE |
| 23 | RENAISSANCE SECURITIES (CYPRUS) LIMITED-NR79707 | MWAKILISHI | STANBIC NOMINEES LIMITED |
| 24 | WATOTO FUND (WATOTO UNIT TRUST SCHEME) | MWAKILISHI | FREDRIC PETER LUSHINGE |
| 25 | BONIFACE MLISI LYIMO | BINAFSI | |
| 26 | ORBIT SECURITIES CO LTD ITF CHRISTOPHER W.HARTLAND-PEEL & GRACIELA M.SCHAR | MWAKILISHI | AMMI JULIAN MWAMUNYI |
| 27 | MTATIRO MGAYA MASIRIKALE | BINAFSI | |
| 28 | EMMANUEL JOSEPH DAFTARI | BINAFSI | |
| 29 | SHABA FAMILY TRUST | MWAKILISHI | SONJA SHABA |
| 30 | MR. HUDSON DAVID MWASAMBUNGU | BINAFSI | |
| 31 | DOMINA CLEMENCE FERUZI | BINAFSI | |
| 32 | SALVATORY PATRICK MLAY | BINAFSI | |
| 33 | SHILLA HATIBU SENKORO | MWAKILISHI | ZAITUNI ABDILIH MDOE |

| NA. | JINA LA MWANAHISA | UWAKILISHI | MWAKILISHI |
|---|---|---|---|
| 34 | WEKEZA MAISHA UNIT TRUST SCHEME | MWAKILISHI | FREDRIC PETER LUSHINGE |
| 35 | EMILIAN P. BUSARA | BINAFSI | |
| 36 | PARESH, HIRJI & KUSUMKANTA HIRJI PATEL | BINAFSI | |
| 37 | DIANA EDWARD MASALLA | BINAFSI | |
| 38 | FRANCISCA ANDREW MOSHI | BINAFSI | |
| 39 | SIWEMA RASHID MPONDA | BINAFSI | |
| 40 | DOLAT ALLY SWEDY | BINAFSI | |
| 41 | SHAFIQ KARIM RATANSI &/OR LINA SHAFIQ RATANSI | BINAFSI | |
| 42 | ESTHER DANIEL MWAIKAMBO | BINAFSI | |
| 43 | IMELDA ALOYCE MARWA | BINAFSI | |
| 44 | STANBIC NOMINEES LTD - IMARA S.P. REID (PTY) LTD | MWAKILISHI | ANDREW MGUNDA |
| 45 | AGGREY SHIFWAYA SAMSON | BINAFSI | |
| 46 | MARTIN JAIRO OKEYO | BINAFSI | |
| 47 | DAUGHTERS OF MARY SINZA | BINAFSI | |
| 48 | BEATRICE GABONE WARANGE | BINAFSI | |
| 49 | DONATUS RICHARD SHAWA | BINAFSI | |
| 50 | MKUVIA YOHANA MAITA | BINAFSI | |
| 51 | STELLA VICTOR NGALAWA | MWAKILISHI | LILIAN NGALAWA |
| 52 | CHRISTINA LUCAS MATERU | MWAKILISHI | MWANAHAMISI YUSUPH JIDAWI |
| 53 | GODFREY KADIOKO MARIKI | BINAFSI | |
| 54 | SIMA GABONE MAFIPA | BINAFSI | |
| 55 | GODFREY DANIEL MARIKI | BINAFSI | |
| 56 | EMMANUEL SAMUEL KIBEYA | BINAFSI | |
| 57 | ALI KHAMISI ALI | BINAFSI | |
| 58 | RICHARD SIDNNEY SHABA | MWAKILISHI | SONJA SHABA |
| 59 | DEBORA ZACHARIA KILELE | BINAFSI | |
| 60 | BEATRICE ZACHARIA KILELE | BINAFSI | |
| 61 | GEORGE FRANK KESSY | BINAFSI | |
| 62 | GRACE ACHA MBEKEM | BINAFSI | |
| 63 | MARION STEPHEN MAFIPA | BINAFSI | |
| 64 | DANIEL ANGASIRIN KWEKA | BINAFSI | |
| 65 | ELIKUNDA ELIREMA MSHANA | BINAFSI | |
| 66 | GODSON RICHARD RULASUMA | BINAFSI | |
| 67 | SAIDA HAMISI MOTTO | BINAFSI | |
| 68 | MARY CASSIAN MBELEKWA | BINAFSI | |
| 69 | SAMWELI DANIEL MAKALA | BINAFSI | |
| 70 | CHARLES PIUS TUNGU | BINAFSI | |

| NA. | JINA LA MWANAHISA | UWAKILISHI | MWAKILISHI |
|---|---|---|---|
| 71 | FRANCOIS  MUNSEMBA MAKASSY | BINAFSI | |
| 72 | RUZIKA NIYO MUHETO | BINAFSI | |
| 73 | LILIAN JAMES HOSEA | BINAFSI | |
| 74 | MEBU MASAMAKI HOFESSY | BINAFSI | |
| 75 | BEATRICE DOMINIC PALLANGYO | BINAFSI | |
| 76 | ABDON PIUS MSHOBOZIE | MWAKILISHI | MSHOBOZI PIUS ABDON |
| 77 | NICHOLAS CHARUKULA NYONYO | BINAFSI | |
| 78 | AGNES NJELDASEFO MARO MOSHA | BINAFSI | |
| 79 | RAJESH JIVANDAS DAVDA | BINAFSI | |
| 80 | GODWIN DAVID NDOSSI | BINAFSI | |
| 81 | IGNACE MARINGA PETER MOWO | BINAFSI | |
| 82 | ADOLFO CARIDADE MASCARENHAS | BINAFSI | |
| 83 | YESSAYA LUDZABIKO MSIGWA | BINAFSI | |
| 84 | MUSHUMBUSI EOGRATIAS KITANKULA | BINAFSI | |
| 85 | JENIFA CHRISTIAN OMOLO | BINAFSI | |
| 86 | STEPHEN MASATO WASIRA | BINAFSI | |
| 87 | JOSEPH SEBASTIAN KIMARYO | BINAFSI | |
| 88 | ROSEMARY RICHARD BGOYA | BINAFSI | |
| 89 | STEPHEN KAJUGA BASIMWAKI | BINAFSI | |
| 90 | MERYNESS JUSTIAN RWEHIKILA | BINAFSI | |
| 91 | ANIN MWIRISHE ULOMI | BINAFSI | |
| 92 | SABITINA IDDI KANIKI | BINAFSI | |
| 93 | HALIMA HUSSEIN KASHUMBA | BINAFSI | |
| 94 | SUSAN MICHAEL WAGNER | BINAFSI | |
| 95 | CLAUDIO MICHAEL MBENA | BINAFSI | |
| 96 | JOHN BENT KIMARO | BINAFSI | |
| 97 | BONIFACE WILLIAM KANYALLA | BINAFSI | |
| 98 | HUMPHREY MELECKZEDECK URASSA | BINAFSI | |
| 99 | KEZIA MISHAEL SWERE | BINAFSI | |
| 100 | FRANCISCA MUKAJUNA NGAIZA | BINAFSI | |
| 101 | GABRIEL GABRIEL MANDARA | BINAFSI | |
| 102 | IRENE DANIEL MAKYAO | BINAFSI | |
| 103 | FATUMA AWADHI MUSHI | MWAKILISHI | ABDUL-HAFIDH HASSAN MARUA |
| 104 | EMMANUEL ELIAS MRITTA | BINAFSI | |
| 105 | JOSEPH SUITING KAWICHE | BINAFSI | |
| 106 | GOLDER ENOCK MAKENGE | MWAKILISHI | ELIDA KASERA MAKENGE |
| 107 | GEOFREY JOSEPH KIWANGA | BINAFSI | |
| 108 | PROSPER ISRAEL TUTINDAGA | BINAFSI | |

| NA. | JINA LA MWANAHISA | UWAKILISHI | MWAKILISHI |
|---|---|---|---|
| 109 | TRIFOSA FRANCIS NATTAY | BINAFSI | |
| 110 | ANNA ANTON MASSAWE | BINAFSI | |
| 111 | EMELIANA SHIZYA NGWALE | BINAFSI | |
| 112 | PROSPER ALBER T MWANGAMILA | BINAFSI | |
| 113 | MATULO YOHANA MMAKA | BINAFSI | |
| 114 | SIHAM SAID AHMED | BINAFSI | |
| 115 | KASSIM OMARY RASHIED | BINAFSI | |
| 116 | AUGUST BENEDICT KOWERO | BINAFSI | |
| 117 | YAHYA ALLY MCHUJUKO | BINAFSI | |
| 118 | JOTHAM KAKURU LUJARA | BINAFSI | |
| 119 | ROSALIA THADDEUS RAGIJE | BINAFSI | |
| 120 | BONIFACE GEOFREY GUNDA | BINAFSI | |
| 121 | MBONI MOHAMED RUTENGWE | BINAFSI | |
| 122 | VICTOR EMILIAN BUSARA | BINAFSI | |
| 123 | JEREMIA JAPHET MUNA | BINAFSI | |
| 124 | LEANDRI STANISLAUS KINABO | BINAFSI | |
| 125 | PETER RWEYEMAMU KASHUSHURA | BINAFSI | |
| 126 | ROSE DAVID SANGA | BINAFSI | |
| 127 | FREDRICK AMBILIKILE MWAKALOBO | BINAFSI | |
| 128 | KHALIFA SEKOUTOURE MNDEME | BINAFSI | |
| 129 | HEMED SEKOUTOURE MNDEME | BINAFSI | |
| 130 | NICHOLAUS ISWESHA MALANDO | BINAFSI | |
| 131 | MARY SAMSON KILEO | BINAFSI | |
| 132 | OSWARD EDWARD RUTALINDWA | BINAFSI | |
| 133 | BERNADETA WARIOBA CHACHA | BINAFSI | |
| 134 | NAFTAL JAPHET SIGWEJO | BINAFSI | |
| 135 | ERASMI DEOGRATIUS MAUSA TARIMO | MWAKILISHI | DEOGRATIUS ERASMI MAUSA |
| 136 | MOHAMED ATHUMANI DOGORI | BINAFSI | |
| 137 | NANA LUCY ALI MNYANI | BINAFSI | |
| 138 | MONICA JASSON NDAMBALA | BINAFSI | |
| 139 | ABDON MSHOBOZI ABDON | MWAKILISHI | MSHOBOZI PIUS ABDON |
| 140 | JULIANA MICHAEL MMASI | BINAFSI | |
| 141 | TRIZA ERASTO META | BINAFSI | |
